Arafa ya Sera

Nambari 42 Julai 2014

Taasisi zilizoshirikiana: Baraza la Kitaifa la Idadi ya Watu na Maendeleo, Wizara ya Afya, na Taasisi ya Kumbukumbu za Idadi ya Watu (PRB)

Uchambuzi wa Mafanikio katika Malengo Kuhusu Idadi ya Watu na Maendeleo – Kenya imepiga hatua gani?

Baada ya Mkutano wa Kimataifa kuhusu Idadi ya Watu na Maendeleo (ICPD), uliofanyika jijini Cairo mwaka wa 1994, kumekuwa na mabadiliko katika msisitizo wa sera na mipango inayohusu usimamizi wa idadi ya watu na uboreshaji wa maisha. Kupitia mkutano huu masuala mbalimbali yalijadiliwa, kama vile kuboresha upatikanaji wa elimu, kupunguza vifo vya watoto na vinavyo husiana na uzazi, na kuboresha upatikanaji wa huduma za afya ya uzazi na kujamiiana.

Mnamo mwaka wa 2000, wakati wa Mkutano wa Milenia, masuala haya na mengine yalijadiliwa na baadaye Malengo nane ya Maendeleo ya Milenia (MDGs) yakatungwa.

Kutokana na mikutano hiyo miwili, baadhi ya malengo yaliyoafikiwa ni elimu kwa wote, uwezeshaji wa wanawake, afya ya watoto na afya ya uzazi. Pia jukumu muhimu la wanawake katika kukuza maendeleo na kwa utekelezaji wa malengo haya, lilitambuliwa. Kwa sababu ya umuhimu wa maadiili haya, Kenya ilitoa ahadi yakuhakikisha kwamba raia wote wanapata elimu ya msingi na kwamba idadi ya vifo vya watoto wachanga, watoto chini ya miaka 5, na vya wanawake wajawazito vitapunguzwa ifikapo mwaka wa 2015.

Tunapo karibia mwaka wa 2015, tunajiuliza je, Kenya imepiga hatua gani kuhusiana na malengo haya? Na kama malengo haya hayajafikiwa kwa sasa, ni mipango gani na mikakati ipi inastahili kutekelezwa ili kuondoa vikwazo na mapungufu yaliyopo? Masuala haya yanachunguzwa kupitia arafa hii.

Mkutano wa Kimataifa Kuhusu Idadi ya Watu na Maendeleo - 1994

Kenya ilikuwa baadhi ya nchi 179 zilizohudhuria Mkutano wa Kimataifa Kuhusu Idadi ya Watu na Maendeleo (ICPD) uliofanyika jijini Cairo mwaka wa 1994. Wajumbe zaidi ya 20,000 kutoka duniani kote walikutana ili kujadili masuala kuhusu idadi ya watu na usimamizi wa idadi ya watu, na wakasisitiza haja ya kuboresha maisha ya watu, hasa ya wanawake. Katika mkutano huo, uwezeshaji wa wanawake na kukidhi mahitaji ya watu kupitia elimu na afya, ikiwa ni pamoja na afya ya uzazi, yalibainishwa kama mambo muhimu ya kuleta maendeleo.

Ilikubaliwa kuwa nchi zina paswa kuunganisha masuala ya idadi ya watu katika mikakati yao ya maendeleo na bajeti. Malengo yote kuhusu masuala haya yaliwekwa pamoja katika Mpango wa Utekelezaji.

Malengo ya Milenia

Malengo yaliyoidhinishwa wakati wa mkutano uliofanywa jijini Cairo mwaka wa 1994 yaliinishwa katika Malengo ya Milenia. Malengo 2 hadi 6 yalitolewa kutoka kwa Mpango wa Utekelezaji / Mikakati wa mkutano huo kama inavyoonekana katika Jedwali 1.

Jedwali 1: Mwingiliano kati ya Malengo ya Mkutano wa Kimataifajuu ya Idadi ya Watu na Maendeleo na yale ya Maendeleo ya Milenia

Malengo ya ICPD – 1994	Malengo ya Milenia – 2000
Elimu kwa wote	2. Kufikia elimu ya msingi kwa wote.
Kupunguza vifo vya watoto wachanga na wale wa chini ya miaka mitano	4. Kupunguza vifo vya watoto.
Kupunguza vifo vya wajawazito	5. Kuboresha afya ya kina mama wazazi.
Utoaji wa huduma za uzazi na afya ya uzazi, ikiwa ni pamoja na upangaji wa uzazi, upatikanaji wa huduma hizi kwa wanaohitaji kwa urahisi na kwa bei nafuu.	6. Kupambana na Ukimwi na virusi vya ukimwi pamoja na kinga.

Aidha, makundi hayo mawili ya malengo yalisisitiza haki za wanawake na uwezeshaji wao. Kielelezo 1 chaonyesha jukumu muhimu linalotimizwa na wanawake katika utekelezaji na mafanikio ya malengo haya.

Kielelezo 1: Wanawake Katikati ya Juhudi za Idadi ya Watu na Maendeleo



Asili: National Council for Population and Development

Jitihada za Kenya katika Utekelezaji wa Malengo ya Milenia na ya ICPD

Sera

Kama saini kwa maazimio na Malengo ya ICPD na ya Milenia, Kenya imebuni sera kadhaa kwa lengo la kuboresha maisha na ustawi wa raia wake. Katika mwaka wa 2000, Kenya ilibuni Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu kwa Maendeleo Endelevu (NPPSD) kwa lengo lakurejelea na kuafikia Mpango wa Utekelezaji wa ICPD na ili uende sambamba na mahitaji ya nchi ya Kenya.

Sera hii liliongoza mipango ya idadi ya watu, afya na maendeleo kutoka mwaka wa 2000 hadi 2010.[1] Katika kipindi hiki, baadhi ya maboresho yalifanywa katika viashiria vya afya ya uzazi na ya watoto. Kwa mfano idadi ya vifo vya watoto wachanga ilipungua kutoka 74 hadi 52 ilhali idadi ya vifo vya wale chini ya miaka mitano ilipungua kutoka 112 hadi 74 kwa kila watoto 1,000 wanaozaliwa wakiwa hai. Katika kipindi hicho, uwiano wa wanawake walio olewa na waliotumia mbinu ya upangaji uzazi uliongezeka kutoka asilimia 39 hadi asilimia 46. Pia, kiwango cha idadi ya watoto kwa kila mwanamke ilipungua kwa wastani kutoka 4.9 hadi 4.6.

Katika mwaka wa 2012, Sera ya Idadi ya Watu kwa Maendeleo ya Taifa ilibuniwa kwa lengo la kuhakikisha kwamba kuna usimamizi bora wa idadi ya watu ili kuwe na mafanikio na maisha bora ya wananchi.[2]

Sera za afya na sheria zilibuniwa na kuidhinishwa katika miaka iliyofuata. Katika mwaka wa 2003, serikali ilipitisha *Sera ya Afya ya Uzazi ya Vijana na Maende*leo *(ARH & D)* kwa lengo la kushughulikia afya ya uzazi ya vijana na haki yao pamoja na masuala mengine ya maendeleo.[3] Ni wakati huu pia ambapo *Sera ya Elimu ya Bure kwa Shule za Msingi (FPE)* ilianza kutekelezwa ili kutimiza lengo la kufanikisha upatikanaji wa elimu ya msingi.

Katika mwaka wa 2007, *Sera ya Taifa ya Afya ya Uzazi* ilibuniwa kwa lengo la kuboresha hali ya afya ya uzazi ya Wakenya wote kwa kuongeza upatikanaji wa huduma za afya ya uzazi, kuendeleza ubora na ufanisi wa utoaji wa huduma, nakuboresha mwitikio kwa mahitaji ya wateja.[4] *Mswada wa Kupiga Marufuku Ukeketaji* ulipitishwa na serikali mnamo mwaka wa 2011. Mswada huu una lengo la kuondoa utamaduni huu unaodhuru wanawake na wasichana.

Katika katiba ya Kenya iliyoidhinishwa mwaka wa 2010, kuna haki mbalimbali zinazolenga kuondoa vikwazo vyovyote vinavyoweza kuzuia wanaume na wanawake kupata huduma za afya na za upangaji wa uzazi.[5] Aidha, serikali ilibuni na inatekeleza *Mfumo wa Sera kuhusu Elimu ya Jamii za Wanao Hamahama* (2010) kwa lengo lakupunguza ujinga na kuboresha elimu miongoni mwa jamii ya wafugaji, hasa kwa wasichana na wanawake.

Programu

Serikali ya Kenya imetekeleza programu kadhaa ili kufikia malengo ya maendeleo. Kuhusu utoaji wa **elimu kwa wote,** serikali ilipitisha kwamba elimu ya shule ya msingi iwe bila malipo. Pia imepunguza gharama ya elimu ya shule za upili na imejitahidi kupanua na kuboresha miundombinu katika ngazi zote mbili. Aidha, baadhi ya mipango ni ya kuhakikisha kwamba wasichana wamo shuleni kila wakati. Kwa mfano, wasichana wanapewa ruhusa kurudi shuleni baada ya kupata mtoto na wasichana kutoka familia maskini hupewa taulo za usafi. Wizara ya Kazi, Usalama na Huduma kwa Jamii inatoa usaidizi kwa shule isiyo rasmi - kama vile utoaji wa elimu kwa watu wazima - ili kuboresha viwango vya elimu miongoni mwa vijana na watu wazima ambao hawamo katika mfumo rasmi wa elimu.

Juhudi za kupungua vifo vya watoto wachanga zimedhihirishwa na Mpango wa Usimamizi wa Magonjwa ya Watoto *(Integrated Management of Childhood Illnesses – IMCI - program).* Kupitia mpango huu, wafanyakazi ambao hutoa huduma za afya wanapewa mafunzo zaidi ili waweze kutathmini watoto na kutambua magonjwa yao ili kuwapa matibabu yafaayo. Programu nyingine mbili zinaenda pamoja na mpango wa IMCI: moja kuhusu ukuzaji wa afya ya watoto shuleni yaani *the Child Health Promotion Program,* na nyingine kuhusu utoaji wa chanjo, yaani *the Kenya Expanded Programme on Immunization-KEPI.*

Kumekuwa na utekelezaji wa programu za **kupunguza vifo vya wajawazito** nchini Kenya kama vile: uboreshaji wa huduma za kliniki, utoaji wa huduma kabla na baada ya kujifungua. Lengo kuu ni wanawake wote wajawazito kutumia huduma hizi. Aidha, Mpango wa Taifa wa Upangaji Uzazi hukuza matumizi ya vifaa au mbinu za upangaji wa uzazi miongoni mwa wanandoa au wanaojamiiana ili kupunguza mimba zisizotarajiwa na hivyo basi kupungua idadi ya uavyaji mimba usiokuwa salama na unao hatarisha maisha.

Serikali na washirika wake wameboresha upatikanaji na uwezo wa kununua huduma za afya ya uzazi kwa kutoa ruzuku ya gharama ya huduma hizi na kuongeza maeneo ya utoaji wa huduma. Baadhi ya huduma hizi, kama vile zile za upangaji wa uzazi, zinapatikana bila malipo yoyote katika vituo vya afya ya umma. Aidha, *Kenya Medical Supplies Agency (KEMSA)* na mawakala wengine wa ugavi, wamehakikisha kwamba bidhaa na vifaa vinavyohitajika ili kutoa huduma hizi, zinapatikana.

Ni mafanikio gani yamefikiwa nchini Kenya kwa sasa?

Elimu kwa wote: Katika mwaka wa 1990, wawili tu kati ya wanafunzi watano walihitimu elimu yao ya msingi. Mnamo mwaka wa 2012, kutokana na utoaji wa elimu ya msingi bila malipo, takwimu hii iliongezeka hadi wanafunzi wanne kati ya watano. Katika kipindi cha kutoka mwaka wa 2002 hadi mwaka wa 2012, viwango vya mpito kutoka shule za msingi kwenda kwa shule za sekondari viliongezeka kutoka asilimia 42 ya wanafunzi hadi asilimia 76. Hii inamaanisha kwamba kati ya wanafunzi zaidi ya 800,000 wanaomaliza shule ya msingi kila mwaka nchini Kenya, 200,000 hawapati fursa ya kuendeleza masomo yao katika shule za upili.

***Vifo vya watoto wachanga na walio chini ya miaka 5*:** Mnamo mwaka wa 1990, kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa hai, kulikuwa na vifo 99 vya watoto chini ya umri wa miaka 5. Kufikia mwaka wa 2003, vifo hivi vilikuwa vimeongezeka hadi 115 kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa hai. Kufikia mwaka wa 2008-09, vifo vilikuwa vimepunguka hadi vifo 74 kwa watoto 1,000 waliozaliwa hai. [6] Zaidi ya nusu ya vifo hivi hutokea katika mwaka wa kwanza wa maisha ya mtoto, kama inavyo onyeshwa na Kielelezo 2. Swali ni je, Kenya itafikia lengo la vifo 33 (vya watoto chini ya miaka 5 kwa watoto 1,000 wanaozaliwa hai) ifikapo mwaka wa 2015?

Kielelezo 2: Mwenendo wa Vifo vya Watoto Wachanga na Walio Chini ya Miaka 5 (1990 – 2009)



Asili: Kenya Demographic and Health Surveys

Vifo vya wajawazito: Wanawake wengi sana hufa nchini Kenya wakati wa kujifungua. Lengo la Milenia ni kupunguza vifo vya wajawazito (vifo vinavyo tokana na matatizo ya mimba na kujifungua) kwa robo tatu ifikapo mwaka wa 2015. Katika mwaka wa 1990, uwiano wa vifo vya wajawazito ulikuwa vifo 590 kwa kila watoto 100,000 waliozaliwa wakiwa hai. Lengo la milenia ni vifo 148 ifikapo mwaka wa 2015. Mwaka wa 2008-09, idadi ya vifo vya wajawazito nchini Kenya ilikuwa katika makadirio ya 488 kwa kila watoto 100,000 waliozaliwa wakiwa hai. Hii inamaanisha kwamba vifo 7,000 vya wajawazito hutokea kila mwaka, na hii ni jambo la kuhuzunisha.

Kielelezo 3: Mwenendo wa Vifo vya Wajawazito (1988 – 2009)



Asili: Kenya Demographic and Health Surveys

Kuhusu ***utoaji wa huduma za afya ya uzazi,*** tathmini kuhusu Utoaji wa Huduma *(Kenya Service Provision Assessment-KSPA)* iliyofanywa mwaka wa 2010 iligundua kuwa tisa kati ya vituo vya afya kumi hutoa mbinu angalau moja ya upangaji wa uzazi. Lakini 4 tu kati ya vituo vya afya 5 hutoa mbinu za kisasa, na 3 kati ya vituo 5 hutoa ushauri kuhusu mbinu za asili, na 1 kati ya 10 hutoa huduma za upasuaji kwa wanaume au wanawake ili kufunga kabisa uzazi.

Utafiti huo pia uligundua kuwa robo tatu ya vituo vya afya hutoa huduma za kliniki, ilhali vituo kidogo zaidi ya nusu hutoa hudumaza baada ya kujifungua. Utafiti huo ulionyesha kuwa chini ya theluthi moja yavituo vya afya hutoa huduma za kujifungua kwa njia ya kawaida, ilhali 1 tu kati ya vituo 20 vya afya, kilikuwa na uwezo wa kutoa huduma za upasuaji kwa akina mama wajawazito.[8] Matokeo haya ya utafiti yanaonyesha kwamba ipo haja ya kuongeza juhudi ili kuboresha upatikanaji wa huduma za afya ya uzazi.

Athari kwa Sera na Mipango

Utendaji wa nchi ya Kenya kuhusu malengo yaliyo buniwa katika miongo miwili iliyopita si ya kuridhisha. Ni vyema serikali na wadau kuhakikisha kwamba watoto wote wanapokamilisha masomo ya shule za msingi wanapata fursa ya kuendeleza elimu yao katika shule za sekondari au kwa taasisi za elimu ya juu. Vifo vya watoto wachanga na wa umri chini ya miaka 5 lazima vipunguzwe kwa zaidi ya nusu, na vifo vya wajawazito vipunguzwe kwa zaidi ya theluthi mbili kabla ya mwaka 2015. Ni vigumu malengo haya ya fikiwe kwa sababu muda uliobaki ni mdogo.

Ruwaza ya mwaka 2030, mpango mkuu wa kiuchumi nchini, inadhani taifa ambayo inaubora wa maisha kwa wananchi wote; wananchi wenye afya, elimu na uwezo wa kuongeza thamani kwa mafanikio ya kiuchumi na ya kijamii. Ndiposa sera za elimu na afya lazima zitekelezwe kikamilifu ili kufikia Malengo ya milenia 2, 4, na 5.

NCPD ni shirika la Serikali linalobuni na kuimarisha sera za idadi ya watu na kushirikisha shughuli zinahusiana kwa ustawi wa maendeleo nchini Kenya.

Shirika la Kitaifa la Idadi ya Watu na Maendeleo
S.L.P. 48994 - 00100, Nairobi, Kenya.
Simu: 254-20-271-1600/01
Kipepesi: 254-20-271-6508
Baruapepe: info@ncpd-ke.org

www.ncpd-ke.org

Jarida hili limechapishwa kwa Ushirikiano wa Watu wa Marekani kupitia Shirika la Marekani la Maendeleo ya kimataifa (USAID) chini ya Mradi wa IDEA (No. AID-0AA-A-10-00009). Yaliyomo kwenye jarida hili yamekusanywa na Shirika la Kitaifa la Idadi ya Watu na Maendeleo (NCPD) na Taasisi ya Kumbukumbu za Idadi ya Watu (PRB) na hayaangazii maoni ya Shirika la USAID wala Serikali ya Marekani.

Mapendekezo

Ili Kenya iweze kuzidisha kasi kwa utekelezaji wa malengo ya maendeleo iliyoafikisha, Baraza la Taifa la Idadi ya Watu na Maendeleo (NCPD) linapendekeza hatua zifuatazo:

- **Elimu kwa Wote:** Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, kwa kushirikiana na washirika katika sekta ya elimu, lazima itie jitihada kwa kutafuta sababu na suluhisho kwa matatizo yanayofanya baadhi ya wanafunzi wasihitimu shule za msingi. Ni bora kuzingatia tofauti kati ya wilaya mbalimbali na kutafuta suluhuhisho zifaazo katika kata mbalimbali. Mbinu hizi lazima ziwe na lengo la kuwezesha wanafunzi wote kuhitimu shule ya msingi na kujiunga na shule za upili au taasisi za elimu ya juu, na hivyo basi kuboresha elimu nchini.

- **Vifo vya Watoto na Wajawazito:** Wizara ya Afya na washirika katika ngazi zote za kitaifa wanapaswa kuupa kipaombele upunguzaji wa vifo hivi. Kwanza kabisa kwa kutambua sababu zinazoleta maafa haya katika kila kata ili kuweka mikakati ifaayo kuzitatua. Serikali ya kila kata kupitia wizara zao za afya inapaswa kuhakikisha kwamba huduma za afya kwa watoto na wajawazito zinapatikana kwa urahisi na kwa bei nafuu.

- **Toa Huduma za Afya kwa Watoto na Wajawazito:** Wizara ya Afya na wadau wakihakikisha kwamba huduma za afya kwa wanawake wajawazito na watoto zinapatikana kwa urahisi, Baraza la Taifa la Idadi ya Watu na Maendeleo itawaunga mkono kwa juhudi zao kupitia kampeni kote nchini kuhusu huduma hizo. Kampeni hizi zitasisitiza faida ya huduma hizi kwa watu binafsi, kaya na taifa.

Hitimisho

Makubaliano yaliyofikiwa katika mkutano wa kimataifa wa ICPD mnamo mwaka wa 1994 na Mkutano wa Milenia mwaka wa 2000, yaliipa nchi zinazoendelea mwelekeo bora katika njia ya kuboresha ustawi wa wananchi wao. Katika utekelezaji wa mapendekezo ya vikao hivi muhimu, Kenya imepiga hatua kubwa, lakini kuna haja ya juhudi zaidi. Serikali ya Kenya na wadau lazima waendelee kutafuta mbinu ya utekelezaji wa malengo haya ya kimataifa na ya maendeleo.

Kumbukumbu

[1]National Council for Population and Development. 2000. *National Population Policy for Sustainable Development*. Nairobi, Kenya.

[2]National Council for Population and Development. 2012. *Population Policy for National Development*. Nairobi, Kenya.

[3]National Council for Population and Development. 2003. *Adolescent Reproductive Health and Development Policy*. Nairobi, Kenya.

[4]Ministry of Health. 2007. *National Reproductive Health Policy*. Nairobi, Kenya.

[5]Government of Kenya. 2010. *The Constitution of Kenya*. Nairobi, Kenya.

[6]Government of Kenya. 2007. *Kenya Vision 2030: A Globally Competitive and Prosperous Kenya*. Nairobi, Kenya.

[7]Kenya National Bureau of Statistics and ICF Macro. 2010. *Kenya Demographics and Health Survey 2008-09*. Calverton, Maryland: KNBS and ICF Macro.

[8] National Coordinating Agency for Population and Development, Ministry of Medical Services, Ministry of Public Health and Sanitation, Kenya National Bureau of Statistics, and ICF Macro. 2011. *Kenya Service Provision Assessment 2010*. Nairobi, Kenya.

©2014 National Council for Population and Development